JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

TANGAZO

UUZAJI WA MITI YA MISAJI KWA NJIA YA MNADA KATIKA SHAMBA LA MITI MTIBWA NA LONGUZA

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) unatarajia kuuza miti aina ya Misaji yenye jumla ya meta za ujazo 13,046 (meta za ujazo 5,099 katika shamba la Miti Mtibwa na meta za ujazo 7,948 katika shamba la Miti Longuza). Mauzo haya yatafanyika tarehe 26 – 27 Agosti, 2019 na 29 – 30 Agosti, 2019 katika shamba la miti Mtibwa na Longuza, mtawalia. Uuzaji katika mashamba yote utaanza saa nne na nusu (4:30) asubuhi. Uuzaji huu utafanyika kwa njia ya mnada kwa kuzingatia kanuni 31 (ii) ya Kanuni za Sheria ya Misitu za Mwaka 2004. Miti hii ya misaji itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.

2. Kampuni au mtu binafsi anayetaka kushiriki mauzo kwa njia ya mnada anatakiwa kuwasilisha maombi kwenye bahasha iliyofungwa kuonesha nia ya kushiriki mauzo kwa njia ya mnada akiambatisha leseni ya biashara, usajili wa kiwanda cha kuchakata magogo kwa mwaka fedha 2019/2020, usajili wa biashara ya mazao ya misitu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN). Aidha, anatakiwa aoneshe jina la shamba, jina la kiunga, namba ya kitalu/vitalu na ujazo anaotarajia kununua kama ilivyo kwenye jedwali namba 1 hapo chini.

3. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika ofisi za meneja wa shamba. Mnada utaendeshwa kwa kufuata Sheria ya Misitu Sura 323.

4. Kila kiunga kitanadiwa peke yake kulingana na bei ya ujazo iliyopo. Hata hivyo, bei ya juu iliyotolewa na mnunuzi wakati wa kufungua bahasha haitazuia wanunuzi wengine kuongeza bei zaidi ya iliyotajwa awali.

5. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unawaalika wanunuzi kutuma maombi yao kwa ajili ya kufanya majadiliano ya kununua miti ya misaji kwa njia ya mnada ambapo mnunuzi anaweza kuchagua viunga vifuatavyo;

JEDWALI Na. 1: ORODHA YA VIUNGA, UJAZO NA BEI YA KIANZIO KATIKA SHAMBA LA MITI LONGUZA

Na.	Kiunga	Meta za ujazo katika kiunga (m^3)	Bei elekezi/M3
A. SHAMBA LA MITI MTIBWA			
A1. TAREHE 26 AGOSTI, 2019 – MNADA KWA WAMILIKI WA VIWANDA VYA SAMANI			
	LR 12A-9	235.37	320,000.00
	FN64-17	221.8	400,000.00
	LR 16B-20	400.31	400,000.00
A2. TAREHE 27 AGOSTI, 2019 – MNADA KWA WAMILIKI WA VIWANDA VYA SAMANI, KUCHAKATA MAGOGO NA WAFANYABIASHARA WENGINE			
	LR 12A	307.57	350,000.00
	LR 12A-1	205.76	400,000.00
	LR 12A-2	229.31	350,000.00
	LR 12A-3	207.14	350,000.00
	LR 12A-4	217.96	350,000.00
	LR 12A-5	144.05	400,000.00
	LR 12A-6	218.68	350,000.00
	LR 12A-7	242.85	350,000.00
	LR 12A-8	210.3	320,000.00
	LR 12A-10	201.01	320,000.00
	LR 12A-11	303.98	320,000.00
	LR 12A-12	103.38	350,000.00
	LR 12A-13	204.31	320,000.00
	LR 12A-14	115.63	350,000.00
	LR 12A-15	193.56	350,000.00
	FN64-16	167.66	400,000.00
	LR 16B-18	303.05	400,000.00
	LR 16B-19	306.31	400,000.00
	LR 16B-21	292.96	400,000.00
	LR 16B-22	66.27	400,000.00
B. SHAMBA LA MITI LONGUZA			
B1. TAREHE 29 AGOSTI, 2019 – MNADA KWA WAMILIKI WA VIWANDA VYA SAMANI			
1	KS12-F5	119.577	720,000.00
2	KS12-F6	106.167	720,000.00
3	KS12-F7	137.51	720,000.00
4	KS12-F8	106.65	720,000.00
5	KS12-F9	114.647	720,000.00
6	KS12-F10	71.421	720,000.00
7	KS12-F11	78.095	720,000.00
8	KS12-F12	96.235	720,000.00
9	KS12-F13	105.192	720,000.00

B2. TAREHE 30 AGOSTI, 2019 - MNADA KWA WAMILIKI WA VIWANDA VYA SAMANI, KUCHAKATA MAGOGO NA WAFANYABIASHARA WENGINE			
1	KS12-A1	386.174	720,000.00
2	KS12-A2	270.214	720,000.00
3	KS12-A3	226.715	720,000.00
4	KS12-A4	240.298	720,000.00
5	KS12-A5	385.657	720,000.00
6	KS12-A6	423.406	720,000.00
7	KS12-A7	432.559	720,000.00
8	KS12-A8	212.985	720,000.00
9	KS12-A9	208.717	720,000.00
10	KS12-A10	281.917	720,000.00
11	KS12-A11	374.753	720,000.00
12	KS12-A12	343.091	720,000.00
13	KS12-A13	387.954	720,000.00
14	KS12-A14	253.717	720,000.00
15	KS12-A15	299.225	720,000.00
16	KS12-A16	222.557	720,000.00
17	KS12-A27	238.775	720,000.00
18	KS12-A28	182.288	720,000.00
19	KS12-A32	518.492	720,000.00
20	KS12-A33	328.671	720,000.00
21	LG8 -10	101.575	630,000.00
22	LG8- 17	430.608	630,000.00
23	LG8 - 22	261.847	630,000.00

6. Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya misaji hataruhusiwa kusafiirisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) ya Mwaka 2004. Kusafirisha mazao ya misitu nje ya nchi ni baada ya kuyachakata kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na 69 la Mwaka 2006.

7. Makampuni na watu binafsi wanakaribishwa kutembelea viunga shambani wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri isipokuwa siku za sikukuu. Meneja wa shamba au msaidizi wake atakuwepo kwa ajili ya maelekezo zaidi.

8. Wanunuzi wanapaswa kuchukua na kusoma masharti ya uvunaji kwa kila shamba. Masharti hayo yanapatikana ofisi za shamba la Mtibwa na Longuza.

9. Bei ya kianzio kwa mita moja ya ujazo imeoneshwa katika Jedwali namba 1 hapo juu ikijumuisha ‘VAT’, ‘CESS’ na ‘LMDA’.

9. Mnunuzi atakayeshinda atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani yote ya ununuzi ndani ya muda wa siku tatu (3) baada ya kushinda. Fedha hizo hazitarudishwa. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya muda wa siku kumi na nne baada ya mnada. Malipo yote yafanyike kwa kupitia mfumo wa makusanyo ya Serikali (GePG) baada ya kupewa Bill ya mfumo kupitia Bank ya NMB au M-pesa. Bili inayoonesha kiasi cha kulipa itatolewa na Meneja wa shamba.

10. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo kwa Meneja wa shamba kama uthibitisho wa malipo si zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

11. Mnunuzi atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya mwezi mmoja baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100.

12. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti zifuatazo za Wakala na Wizara: www.tfs.go.tz, na www.mnrt.go.tz

13. Maombi yote yawasilishwe siku ya mauzo kabla ya saa 4:00 asubuhi. Wanunuzi watakaochelewa kuwasilisha maombi yao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika majadiliano ya mauzo.

limetolewa na

MTENDAJI MKUU
S.L.P 40832
DAR ES SALAAM